



Taarifa Kuhusu Upigaji Kura wa Wakazi Wote Halali wa Jiji la Burlington

Hati ya Jiji la Burlington, Sheria za 1949, Nambari 298

Mnamo Machi 2023, wakazi wa Burlington walipiga kura kutekeleza sheria ya Upigaji Kura wa Wakazi Wote Halali. Kura hiyo ilishinda kwa uungaji mkono wa 68%. Kuwaruhusu Wakazi Wote Halali kupiga kura katika chaguzi zetu za eneo huwawezesha wanajamii wanaoishi, kufanya kazi na kulipa ushuru ndani ya Burlington kutoa maoni yao.

Je, Upigaji Kura wa Wakazi Wote Halali ni Nini?

Upigaji Kura wa Wakazi Wote Halali huwaruhusu wakazi wa muda wote wa Burlington ambao wanaishi hapa kihalali lakini hawana uraia kamili wa Marekani kupiga kura katika chaguzi za eneo. Kwa mfano, watu wanaomiliki hati rasmi ya makazi ya kudumu (green card), wakazi wenye vibali vinavyostahiki vya kazi au wapokeaji wa Msamaha wa Muda Dhidi ya Kufukuzwa Nchini kwa Watu Waliowasili Nchini Wakiwa Watoto (Deferred Action for Childhood Arrivals, DACA) wote wanastahiki kuijandikisha kupiga kura katika changuzi za eneo.

Je, Wakazi Halali wanastahiki kupiga kura katika vipengee vipi?

Wakazi Halali ambao si raia wa Marekani, wanastahiki kupigia kura:

- Maafisa wanaochaguliwa kwa kupiga kura wa Jiji la Burlington na Wilaya ya Shule ya Burlington, ikiwa ni pamoja na Meya, Madiwani wa Jiji, Makamishna wa Shule na maafisa wa uchaguzi wa jiji
 - Maswali yoyote kuhusu Jiji la Burlington au Wilaya ya Shule ya Burlington
- Wakazi halali ambao si raia wa Marekani hawaruhusiwi kupiga kura katika chaguzi za jimbo au shirikisho.

Je, wapiga kura ambao ni Wakazi Halali wanastahiki kuwania ofisi za jiji?

Ndiyo, baada ya mkazi kuandikishwa kupiga kura, mtu huyo anaweza kuwania ofisi za jiji.

Je, Mkazi Halali anaweza kuijandikisha kupiga kura vipi?

Jiandikishe kupiga kura kwa kujaza Fomu ya Kuijandikisha Kama Mpiga Kura ya Wakazi Wote Halali wa Jiji la Burlington (inapatikana mtandaoni katika

<https://www.burlingtonvt.gov/CT/Voter-Registration-Info>), nauirudishe kwa Ofisi ya Mhazini wa Karani katika 149 Church Street, Burlington, VT 05401. Wakazi halali pia wanaweza kuijandikisha kupiga kura katika eneo lao la kupiga kura katika Siku ya Uchaguzi.

Una Maswali?

Piga simu kwa ofisi ya Mhazini wa Karani wa Burlington kwa 802-865-7000 au utume barua pepe kwa burlingtontownclerk@burlingtonvt.gov